JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Barabara ya
Kilimatinde Cheyo,
S.L.P. 1020,
45112
TABORA,
Barua Pepe: rbctabora@pccb.go.tz.
TANZANIA.
www.pccb.go.tz

TAARIFA YA UTENDAJI KAZI APRILI 2020 HADI JUNI 2020

TABORA – JULAI 17, 2020

TAKUKURU Mkoa wa Tabora kwa kipindi cha Aprili 2020 hadi Juni 2020 imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na 11/2007 kama yalivyoainishwa katika kifungu cha 7.

Utekelezaji wa majukumu hayo umefanyika kwa kuendelea kufanyia kazi malengo tuliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2019/2020 katika madawati ya Uchunguzi, Elimu Kwa Umma na Uzuiaji Rushwa.

ELIMU KWA UMMA

Katika upande wa kuelimisha jamii ili ishiriki kivitendo katika mapambano dhidi ya rushwa, elimu ilitolewa kwa makundi mbalimbali ikiwemo klabu za wapinga rushwa katika shule za msingi, sekondari na vyuo, watumishi wa umma na mashirika ya Serikali nayo yalielimishwa kuhusu madhara ya rushwa na namna ambayo wanapaswa kupambana nayo.

Kazi ambazo zimefanyika ni pamoja na:-

- Semina **13,**
- Uandaaji wa makala **07**,
- Mikutano ya hadhara na mijadala ya wazi **16,**
- Utoaji wa habari na vipindi redioni **03.**
- Kuimarisha na kufungua vilabu vya wapinga rushwa **02.**

UZUIAJI RUSHWA

Dawati la uzuiaji rushwa lina majukumu makuu mawili ambayo ni ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa mifumo. Majukumu yote haya mawili yana lengo la kuweza kubaini uwepo wa viashiria au vitendo vya rushwa ili kuweza kuchunguza au kushauri mamlaka husika namna bora ya kuziba mianya ya rushwa.

Katika kipindi cha Aprili – Juni 2020 TAKUKURU Mkoa wa Tabora imeendelea kufuatilia maazimio mbalimbali yaliyotokana na chambuzi za mifumo zilizofanyika katika kipindi cha Julai 2019 –Machi 2020 ili kuhakikisha kuwa wadau wanatekeleza majukumu yao kama yalivyoainishwa katika vikao vya makubaliano. Ufuatiliaji uliofanyika ni pamoja na maazimio katika maeneo yafuatayo:

- Manunuzi ya Umma kwenye Sekta ya Afya yanayotekelezwa kupitia Force Account,
- Ufuatiliaji katika matumizi ya fedha za ruzuku za Serikali zinazotolewa kwa shule za msingi (Capitation Grants),
- Uchambuzi wa mifumo ya Malipo ya wakulima wa Tumbaku na Ufuatiliaji wa Matumizi ya Mashine za kielektroniki (POS) katika ukusanyaji wa mapato.

Aidha, katika eneo la ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ujenzi wa majengo na ukarabati wa miundombinu ya shule ya sekondari Milambo unaogharimu Sh. 522,072,250.17 umefanyika.

UCHUNGUZI NA MASHTAKA

Katika kipindi husika, TAKUKURU Mkoa wa Tabora imepokea jumla ya malalamiko 54 ambayo kati yake 29 yalikua na viashiria vya Rushwa, na 25 hayakua na viashiria vya Rushwa na watoa Taarifa 13 walipewa ushauri kulingana na malalamiko yao na malalamiko 12 yalihamishiwa kwenye idara zingine kwa ufatiliaji zaidi. Pia katika dawati la uchunguzi kazi zifuatazo zilifanyika :

- Tumekamilisha majalada ya uchunguzi kumi na nne (14)
- Tumefungua kesi mpya tano (5) Mahakamani
- Majalada Manne (4) yalipata kibali cha DPP
- Kesi (4) zimetolewa maamuzi na kushinda
- Jumla ya mashauri ishirini na moja (21) yanaendelea mahakamani

FEDHA ZILIZOOKOLEWA

Kuanzia Aprili 2020 hadi Juni 2020 TAKUKURU Mkoa wa Tabora imefuatilia na kuokoa fedha jumla ya Shs. 74,533,192/= (**milioni sabini na nne laki tano thelathini tatu mia moja tisini na mbili**) katika maeneo mbalimbali ikiwemo kwenye miradi ya maendeleo, vyama vya ushirika na kwenye mikopo umiza kwa waliokuwa watumishi wa umma.

Kati ya fedha zilizookolewa TAKUKURU imefanikiwa kurejesha fedha jumla ya shilingi 24,640,000/= zilizotokana na mikopo umiza (mikopo inayotolewa bila kufuata taratibu).

Wakopeshaji waliwataka wastaafu kulipa riba ya asilimia 500 ndani ya miezi minne. Mfano aliyekopeshwa Shs 6,000,000/= alitakiwa kurejesha shs 30,000,000/= ndani ya miezi minne, jambo hili ni kinyume na sheria na taratibu za nchi.

TAKUKURU ilifanya uchunguzi juu ya utolewaji na ulipwaji wa mikopo hiyo na kubaini uonevu na ukiukwaji mkubwa wa taratibu za ukopeshaji hali iliyopelekea kuwaelekeza wakopeshaji hao kurejesha fedha walizochukua kama malipo ya mikopo na riba. Sehemu ya fedha zilizorejeshwa na wakopeshaji kiasi cha Shs 24,640,000/= kati ya shs 76,000,000/= wanazotakiwa kurejesha wakopeshaji leo hii zinarejeshwa kwa walimu wastaafu waliokumbwa na kadhia hii.

Aidha, TAKUKURU Mkoa wa TABORA ilifanikisha urejeshwaji wa Shs. 850,000/= kwa wananchi wawili:

- **Wa kwanza** ni ndugu HAMIS SAAD ambaye ni mlemavu wa macho (Haoni), aliyerejeshewa shs 300,000/= zilizochukuliwa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Intonjanda Kata ya Itonjanda Manispaa ya Tabora wakati wa kuuza kiwanja chake. Mwenyekiti huyo alidai na kulipwa Shs 300,000/= kwa madai kuwa ni kwa ajili ya maendeleo ya kijiji lakini hakutoa risiti na Mzee HAMIS SAAD amekua akifatuatia risiti ya fedha hizo tangu mwaka 2017 mpaka alipotoa taarifa TAKUKURU tarehe 19.06.2020 ambapo taarifa ilifanyiwa uchunguzi na kupelekea mzee huyo kurejeshewa fedha zake na Mwenyekiti huyo chini ya usimamizi wa TAKUKURU Tabora.

- **Wa Pili** ni kutoka Kijiji cha Mwitikila Kata ya Goweko Wilaya ya Uyui Bw. Timbo Jilasi alirejeshewa Shs 550,000 alizodaiwa na Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwitikila ili amruhusu kuendelea kulima kwenye shamba lake baada ya kudaiwa kuwa shamba analolima ni njia ya ng'ombe kwenda kwenye josho.

MIKAKATI TULIYOJIWEKEA KWA KIPINDI CHA MWAKA MPYA WA FEDHA JULAI 2020 - JUNE 2021

TAKUKURU mkoa wa Tabora utawekwa mkazo katika kuelimisha na kuzuia vitendo vya rushwa katika jamii hasa Rushwa kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Madiwani, Wabunge na Rais utakaofanyika Oktoba 2020. Hii ni katika kuhakikisha kuwa wananchi na wagombea hawajihusishi na vitendo vya Rushwa na wanapatikana viongozi wenye maadili.

TAKUKURU mkoa wa Tabora, tunawataka wananchi wote na wanasiasa kufuata taratibu na sheria za nchi. Yeyote atakayebainika kujihusha na uvunjifu wa sheria na vitendo vya rushwa kabla, wakati na hata baada ya uchaguzi hatutasita kumchukulia hatua kali za kisheria, kwa kuwa inawezekana tukafanya uchaguzi usiogubikwa na vitendo vya rushwa.

Niwakumbushe wananchi wa mkoa wa Tabora tukirubuniwa na wanaogombea nafasi ya uongozi kwa kutupa rushwa nasi tukakubali athari zake ni kubwa sana kwani hatutapata maendeleo stahiki. Hao waliochaguliwa baada ya kutupa rushwa watataka kurudisha hela walizotumia wakati wa uchaguzi. Tusiwakubalie watununue kwa kutupa vizawadi visivyo sawa na utu wetu.

Wananchi wa Tabora tukumbuke*, KURA YAKO NI MAENDELEO YAKO USIPOKEE WALA KUTOA RUSHWA ILI UCHAGUE AU KUCHAGULIWA*

Nawashukuru wananchi wote wa Mkoa wa Tabora kwa ushirikiano mnaotoa kwa TAKUKURU, tuendeleze moyo huo na tuwafichue na kutoa taarifa juu ya vitedo vya rushwa vinanvyojitokeza katika maeneo yetu. Nanyi wadau wetu wana habari asanteni sana kwa kazi yenu nzuri ya kuuhabarisha umma kuhusu madhara ya Rushwa.

Asanteni sana

Imetolewa na:

Musa Chaulo
MKUU WA TAKUKURU (M) TABORA